**KISWAHILI KIDATO CHA TATU**
**KARATASI YA PILI 2019**
**MWONGOZO**

1. **Ufahamu**

(a) **(i)** Matabaka ya kitawala
(ii) Ubinafsi
(iii) Ukandamizaji wa wananchi
3x1=alama 3

(b) (i) Hali ya magavana kupigania njia za kujilimbikizia mali.
(ii) Dhana ya ukabila-watu wanajitambua kulingana na jamii/ukoo wao.
2x1=alama 2

(c) Watu kujitambua kulingana na koo zao ni sawa na moto kama uadui utachipuka kati ya watu wa jamii moja. Kwa mfano Waembu na Wambere.

Hali hii inaweza kusababisha maafa kama vile vita vya kiukoo. (alama 3)

(d) Katika shamba la wanyama, nguruwe anayeitwa Old Major aliandika amri saba ambazo zitihakikisha kuwa rasilimali zote katika shamba zingegawanywa kwa wanyama wote. Baada ya mapinduzi wanyama waliochukua hatima ya uongozi waliendeleza ubinafsi uliosambaratisha mfumo wa uongozi.

Kwa sasa hali hii inaendelea Kenya ambapo viongozi waliochaguliwa kuwakilisha kaunti/majimbo wanakandamiza raia kwa kuwatoza kodi, wanaendeleza ubepari n.k. (alama 3)

(e) Kila uovu kama vile ulafi, wizi n.k unaoendelezwa na viongozi magavana unasingiziwa ugatuzi. (alama 2)

(f) (i) Inaakisi-inaashiria
(ii) Mizozo ya kiukoo-ugomvi/vita/ghasia za kikabila, watu wanaotokana na nasaba moja.(alama 2x1= alama 2

**Adhabu**:
(i) Kila kosa la sarufi litokeapo mara ya kwanza liadhibiwe kwa kutozwa (½ maki hadi makosa 6.
(ii) Kila kosa la hijai litakeapo mara ya kwanza liadhibiwe kutozwa (½ maki Hadi makosa 6.


Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – NairobTel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**UFUPISHO**

(a) (i) Uhaba wa nafasi za kazi umeendelea kushika kasi.
(ii)Serikali inatoa wito kwa watu kujiibidiisha kujiajiri badala ya kungojea ajira.
(iii)Kuna vikwazo vinavyowafanya watu kutotaka kuanzisha biashara.
(iv)Baadhi ya watu hawataki kuanzisha biashara kwa hofu ya kutofaulu.
(v)wengi wanaogopa kuweka pesa kwenye biashara zisizowafaidi baadaye.
(vi)kuna ukosefu wa pesa za kununulia mtaji.
(vii)vijana wengi hawana hela za kununua vifaa wala kulipa kodi ya nyumba za kazi.
(viii) Hawapati mikopo kwa kukosa wadhamini.
(ix) mashirika ya kutoa mikopo yanadai riba kwa wadeni wao.
(x) jambo hili huwafisha moyo wawekezaji wadogowadogo.
(xi) Baadhi ya watu hudharau kazi za kuajiri kwa kukosa pato nono.

Zozote 10 x 1 =alama 10.

(b) (i) usalama ni muhimu kwa ufanisi wa biashara.
(ii) Watu hawataki kuanzisha biashara bila usalama
(iii) Visa vya wizi ujambazi huzuia watu kuanzisha biashara katika mitaa yenye kodi ya chini.
(iv) Serikali inawashawishi wananchi kujiajiri ili kupunguza uhaba wa kazi.
(v) Viongozi wanapaswa kuwapa vijana mikopo yenye malipo nafuu.
Serikali ihakikishe hili limetimia.
(vi) Vilevile iwalinde wafanyabiashara wadogowadogo dhidi ya ushindani wa bidhaa kutoka nje kwa kuzitoza ushuru mkubwa.

a-Alama 9
b-Alama 4
utiririko 2
jumla 15

**Adhabu**

(i) Kila losa la sarufi litokeapo mara ya kwanza liadhibiwe kwa kutozwa ½maki hadi makosa 6.
(ii) Kila kosa la hijai litokeapo mara ya kwanza liadhibiwe kwa kutozwa ½maki hadi makosa 6.
(iii) Mtahiniwa hana idhini kuzidisha idadi kwa maneno 9. Akipita kiwango hiki atozwe ½maki kwa kila maneno matano matano.


Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – NairobTel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**MATUMIZI YA LUGHA**

(a)

(i) Silabi ni kipashio cha kimatamshi ambacho kimsingi ni kikubwa kuliko sauti.
Tamko katika mfumo wa sauti.

(ii) Ngwa, ngwe, mbwa-yoyote (alama 1)

(b)

| S | | | | |
|---|---|---|---|---|
| KN | | KT | | |
| N | S | T | N | r |
| Mgeni | Ambaye amewasili | ni | mtoto | wangu |

8x½=4

(c) (i) karibu na, kando ya ukingoni mwa, mbele ya, pembeni mwa, n.k.
Hakiki sentensi. (alama 2)

(ii)Ndiye k.m
Huyu ndiye mwalimu. Hakiki (alama 2)

(d) (i) Mwanafunzi-kitondo
(ii)Mtihani-kipozi
(iii)Kalamu –ala (alama 3)

(e) Huduma (alama 1)

(f) (i) Mwalimu ameweka kitabu kando.
(ii)Mwalimu ametukabidhi kitabu. (2 x 1=alama 2)

(g) Bi Tolo alienda kwa Batu kuomba mapambo ya kujirembesha, akamwambia."Ndugu yangu, najua langu ndilo lako na lako ndilo langu. Naomba uniazime marashi"(alama 3)

(h) (i) Mtoto alipigwa kwa rungu Hakiki
(ii)Alipata hamsini kwa mia Hakiki (alama 2)


Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – NairobTel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

(i) (i) Mwalimu aliniadhibu kijeshi.
Aliongea kitoto (alama 1)

(ii)Wapo, ikiwa, kama,ukitaka
Hakiki sentensi (alama 1)

(j) Punda waliumia kwato zao walipokuwa wakipita nyuani. (alama 2)

(k) Wao wasingetuazima kitabu tusingemaliza kazi kwa wakati. (alama 2)

(l) Huyo mtoto hawezi kusomesheka Historia. (alama 2)

(m) (i)Niliosha vyombo
(ii)Nilikimbia sokoni –vishazi huru

(n) Kipya kizuri hata kikiwa kidonda (alama 2)

(o) (i) Mwanzoni mwa sentensi
(ii)Majina ya watu
(iii)Siku za wiki, miezi n.k.
(iv)Masomo.k.m.Hisabati,Kiswahili n.k.
Yeyote 4 x ½ (alama 2)

(p) K.m. Niliyeitiwa. Hakiki(alama 2)
-Ni –Nafsi
-li-wakati
-Ye-kirejeshi
-it-mzizi
iw-kauli
a-kiishio
(au sentensi nyingine yoyote iliyo sawa).

(q) (i) rejea ulipotoka
(iii) Nguo kuwa fupi
(iv) Adhibu mtoto zozote 2x1=alama 2

**ISIMU JAMII (alama 10)**

(a) **(i)** chanzo cha Kiswahili ni Jamhuri ya kidemokrasia ya Kongo.
(ii) Kiswahili ni tokeo la maingiliano baina ya waafrika na waarabu.
(iii) Kiswahili kilitoka uarabuni/ni lugha ya kiarabu
(iv) Kiswahili ni lugha ya kibantu
(i)Mitazamo mitatu ya kwanza haina mashiko.


Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – NairobTel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

(ii)Mtazamo wa mwisho una mashiko kwani msamiati wa Kiswahili na wa kibantu unakaribiana sana.(3x2=alama 6

(b) (i)Ni kitambulishi cha utaifa.
(ii)Lugha ya taifa
(iii)Lugha rasmi
(iv)Chombo cha kutolea elimu.
(v)Chombo cha mawasiliano
(vi) Nyenzo ya kuwaunganisha watu wenye asili mbalimbali.
Zozote 4 x 1=alama 4

(vii) Kila kosa la sarufi litokeapo mara ya kwanza liadhibiwe kwa kutozwa ½ maki hadi makosa 6

(viii) Kila kosa la sarufi litokeapo mara ya kwanza liadhibiwe kwa kutozwa ½maki hadi makosa 6.

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.**


Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – NairobTel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com